

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**



**WARAKA NAMBA MOJA WA MWAKA 2021 WA KUTOKUZUIA MAITI NA KUWEKA  
UTARATIBU WA KULIPIA GHARAMA ZA MATIBABU NA MADENI KWA MIILI.**

**SEPTEMBER, 2021**

## **1.0 UTANGULIZI**

Kufuatia malalamiko ya wananchi kuzuiliwa kuchukua miili ya marehemu wao katika vyumba vya kuhifadhi maiti katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya nchini. Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kuandaliwa kwa utaratibu bora wa kulipia matibabu na kuruhusu miili ya marehemu kuchukuliwa bila usumbufu.

Kufuatia agizo hilo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeandaa mwongozo wenye maudhui na maelekezo yaliyojikita katika maeneo yafuatayo;

- a) Kulipia gharama za matibabu ili kuzuia malimbikizo ya madeni kwa wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.
- b) Kuruhusu ndugu kuchukua mwili wa marehemu katika vituo vya kutolea huduma za afya aliyekuwa na deni la matibabu na namna ya kulipia deni baada ya mwili kuchukuliwa.

## **2.0 MAELEKEZO MAHUSUSI YA MWONGOZO HUU.**

### **2.1 Utaratibu wa kulipia gharama za matibabu ili kuzuia malimbikizo ya madeni kwa wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.**

Gharama za matibabu ya wagonjwa zitalipwa kwa utaratibu uliopo katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya. Aidha, kuzingatia gharama za matibabu bila kuathiri ubora wa huduma inayotolewa kwa mgonjwa aliyeletwa na ndugu au aliye fika kituo cha kutolea huduma peke yake, utaratibu ufuatao utatumika;

2.1.1 Mgonjwa aliyefikishwa kituo cha kutolea huduma akiwa hajitambui na hana ndugu aliyeambatana naye atapewa kibali cha muda na Afisa Ustawi wa Jamii au Afisa anayeshughulikia huduma za ustawi wa jamii ili matibabu kuendelea wakati ndugu wanasubiriwa.

2.1.2 Mgonjwa aliyefikishwa kituo cha kutolea huduma akiwa hajitambui na hana ndugu aliyeambatana naye na baadae ndugu wa mgonjwa kujitokeza na kubainika

kwamba hawana uwezo wa kulipia gharama za matibabu. Ndugu wa mgonjwa watapaswa kufuata taratibu za msamaha kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007. Aidha, kituo cha kutolea huduma kinapaswa kutoa utaratibu wa upatikanaji wa msamaha wa matibabu.

2.1.3 Mgonjwa aliyefika akiwa anajitambua katika kituo cha kutolea huduma anatakiwa kuwa na vielelezo kutoka ofisi ya mtendaji wa serikali ya mtaa anapoishi vinavyoonesha kuwa hana uwezo wa kumudu gharama za matibabu na kuthibitishwa na Afisa ustawi wa jamii au Afisa anayeshughulikia huduma za ustawi wa jamii katika kituo cha kutolea huduma. (**Mfumo wa rufaa kwa wagonjwa lazima uzingatiwe**).

2.1.4 Kwa mgonjwa ambaye mwanzoni alikuwa na uwezo wa kulipa gharama, lakini akashindwa kuendelea kugharamia matibabu akiwa ndani ya kituo cha kutolea huduma za afya, utaratibu wa kupata msamaha kwa mujibu wa mwongozo utafuatwa.

2.1.4 Kila kituo cha kutolea huduma za afya kiwe na Afisa Ustawi wa Jamii au Afisa aliyeteuliwa kwa ajili ya kushughulikia huduma za ustawi wa jamii.

2.1.5 Kila kituo cha kutolea huduma za afya kiweke utaratibu wa malipo ya awali au baada ya huduma kutolewa, na kuandaa ankara za malipo ya huduma za matibabu na kuwapa wagonjwa au ndugu wa mgonjwa kila siku ili kupunguza malimbikizo ya gharama za matibabu.

2.1.6 Huduma kwa wagonjwa waliolazwa itazingatia vipengele 2.1.1 mpaka 2.1.5.

### **3.1 Utaratibu wa kuchukua mwili wa marehemu katika vituo vya kutolea huduma za afya.**

Taratibu za uchukuaji mwili wa marehemu zitazingatia Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Kuhifadhi Maiti wa Mwaka 2020 pamoja na gharama za huduma zilizotolewa. Pia, yafuatayo yatazingatiwa;

3.1.1 Kwa mgonjwa aliyefia hospitalini, maiti itaanza kulipiwa baada ya kupita saa 24 (siku moja) tangu mwili kupokelewa chumba cha maiti. Kwa maiti


aliyeletwa hospitalini kwa ajili ya kuhifadhi, gharama zitaanza kulipwa mara tu anapofikishwa chumba cha maiti.

- 3.1.2 Iwapo marehemu alikuwa anahudumiwa kwa msamaha wa matibabu, ndugu waruhusiwe kuchukua mwili wa marehemu.
- 3.1.3 Iwapo marehemu alikuwa anachangia gharama za matibabu na mauti yamemfika akiwa na deni la gharama za matibabu, ndugu aruhusiwe kuchukua mwili baada ya kufanya malipo.
- 3.1.4 Iwapo ndugu wa marehemu hawatakuwa na uwezo wa kulipa deni pale mgonjwa atakapokuwa amefariki, ndugu wataingia makubaliano ya maandishi na kituo cha kutolea huduma ya namna ya kulipa deni na waruhusiwe kuchukua mwili.

#### **4.0 HITIMISHO**

Timu za usimamizi wa huduma za afya za vituo vya kutolea huduma pamoja na Timu za Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya ngazi ya Halmashauri (CHMT) na Mikoa (RHMT) zisimamie ipasavyo utekelezaji wa Mwongozo huu. Aidha, msisitizo uwekwe katika kuhakikisha kila mwananchi ana jiunga na Bima ya Afya.

Umetolewa na;

  
Prof. Abel N. Makubi  
**KATIBU MKUU- AFYA**  
04/10/2021